M-AKIBA

Okoa Pesa, Ekeza Pesa, Jenga Kenya...

BONDI REJAREJA YA M-AKIBA

MKM

(Maswali Ya Mara Kwa Mara)

1. Bondi ni nini?

Bondi ni mkopo ambao mwombaji anapewa na mkopeshaji. Mwombaji anaahidi kumlipa mkopeshaji kila baada ya miezi sita. Mwombaji anaahidi pia kulipa pesa zote alizopewa na mkopeshaji mwishoni mwa kipindi walichosikizana.
Bondi hulipwa kwa zaidi ya mwaka mmoja; mwombaji hutumia pesa hizo kutekeleza majukumu mahususi.

2. Ni nini maana ya Bondi ya mauzo ya M-Akiba?

Bondi ya mauzo ya M-Akiba hutolewa na serikali ya Kenya ili ipate pesa za kufadhili miradi ya miundomsingi.

3. Ninaweza kununua Bondi ya M-Akiba kwa njia gani?

Kuna njia mbili ambazo unaweza kununua M-Akiba; kupitia akaunti ya simu au kupitia Pesalink.

- Weka angalau Kshs.3,000 kwenye akaunti ya simu; hakikisha kuwa umejumuisha ada za kutuma. Piga simu kwa *889# na ufuate maagizo yaliyopo.

- Katika mfumo wa PesaLink, hakikisha kwamba umejisajili kwa M-Akiba ama ubonyeze *889# na kisha ufuate maagizo. Nenda kwenye chaguo la malipo, kisha chagua PesaLink na tena uchague mfumo wa benki utakaokupendeza halafu chagua sehemu ya 'tuma kwa chaguo la simu', kisha ingiza **889** kama akaunti yako ya benki, halafu weka thamani ya bondi yako unayotaka kununua, kisha ingiza nambari yako ya **kitambulisho** katika kisanduku cha maelezo ulichoandaliwa. Tuma maelezo hayo, na baada ya hapo utapokea ujumbe wa kukupatia hakikisho la kupokelewa kwa maelezo yako kutoka kwa benki yako pamoja na utapokea ujumbe mwingine kutoka CDSC ukikupatia hakikisho la ununuaji wako wa bondi.

Sasa uko tayari kuhifadhi pesa ukitumia Bondi ya M-Akiba.

4. Kima cha chini cha Bondi ambacho ninaweza kununua wakati wa ofa ni kiasi gani?

kima cha chini cha Bondi ambacho mwekezaji anaweza kununua kwa kila shughuli ya malipo ni Bondi ya Kshs.3,000. Baadaye, unaweza kununua kwa vipimo vya Kshs.500.00 kila siku hadi pesa zote za ofa zitakapokamilika.

Hakuna vikwazo kuhusu kima ambacho mwekezaji anaweza kununua katika soko la hisa.

5. Kuna kiwango ambacho ninastahili kununua kwa siku?

Ukichagua kutumia akaunti ya simu, kima cha juu ambacho kila mwekezaji anaruhusiwa kila siku ni Kshs.140,000. Hata hivyo, ukitumia Pesalink, Kiwango cha juu cha pesa ni Kshs. 999,999 kila mara unaponunua bondi. Kiwango cha uhawilishaji wa pesa kwa siku unategemea na salio la pesa kwenye akaunti yako ya benki.

6. Ni kiwango kipi cha pesa ambacho serikali inalenga kupa kupitia Bondi ya mauzo ya M-Akiba?

Serikali inanuia kukopa shilingi bilioni 4.85 kupitia Bondi ya M-Akiba. Serikali ilipandisha jumla ya Milioni 150 katika ''Ofa Maalum'' iliyokuwa imetolewa mnamo 23 Machi huku ikiwa na tarehe ya kufunga ya ununuaji huo mnamo 7 Aprili lakini ilinunuliwa kwa kiwango cha ziada na kulazimu kufungwa kwa bondi hiyo siku mbili kabla.

7. Serikali itanilipa lini pesa zangu?

Pesa za Bondi zitakuwa tayari baada ya miaka mitatu (3); hii inamaanisha kuwa utalipwa pesa ulizoweka awali ambazo tunaziita "kiasi cha msingi" baada ya miaka mitatu, mbali na riba utakayopokea kila mwaka kwa miaka mitatu.

8. Kiwango cha riba ya Bondi ya M-Akiba ni kiasi gani?

Kiwango cha riba cha Bondi hii ni 10% kwa kila mwaka na hakibadiliki.

9. Nitalipwa riba yangu mara ngapi?

Riba italipwa mara mbili kwa mwaka (baada ya kila miezi sita) katika miaka mitatu inayofuata.

10. Kuna faida gani ya kuwekeza katika Bondi ya mauzo ya M-Akiba?

- Bondi ya M-Akiba ni njia salama ya kuweka akiba kwa sababu inalindwa na hazina ya serikali
- Inaweza kupatikana kwa shilingi 3,000/- pekee
- Ni chanzo imara cha kupata riba inayolipwa baada ya kila miezi sita
- Riba unayopata haitozwi kodi. Hii ina maana kuwa, hutalipia kodi yoyote unapopokea riba hiyo
- Uweza kujiondoa. Yaani unaweza kuuza Bondi yako ukiwa mahali popote kuanzia 9.00 am hadi 3.00 pm
- Ni nji bora ya kuhifadhi pesa ambazo utatumia baadaye na ina faida kubwa
- Ni rahisi kuipata na kuiuza kwa sababu inatumia simu.
- Ni njia salama na ya faragha
- Unaweza kuipata ukiwa mahali popote wakati wowote.

11. Ni nani anaweza kununua Bondi?

Mkenya yeyote aliye na simu ya mkononi na akaunti ya simu ya mkononi anaweza kununua Bondi hii.

12. Bondi ya M-AKiba inatofautiana vipi na Bondi zingine zilizotolewa awali na serikali?

Kima cha chini cha kuwekeza ni shilingi 3,000/- ikilinganishwa na shilingi 50,000 utakazohitaji ili kununua Bondi zingine. Kwa hivyo M-Akiba inaweza kununuliwa na mtu yeyote. Pia ni mbinu ya kwanza kabisa ya kununua Bondi kupitia simu ya mkononi.

13. Kuna faida gani kununua Bondi ya M-Akiba?

Mbali na kuwa mbinu bora ya kuweka akiba inayopatikana kwa Mkenya wa kawaida na iliyo na riba kubwa ya 10% kwa kila mwaka, mbinu hii pia itakupa uwezo wa kufikia kiwango cha dhahabu cha bidhaa zinazonunuliwa katika soko la hisa, ambacho awali hungeweza kukifikia.
Wewe utashiriki katika kujenga taifa moja kwa moja wakati pesa za Bondi zitatumika kuunda miundomsingi ya nchi kwa hivyo unachangia katika kuendeleza uchumi na maisha bora ya Wakenya popote walipo.

14. Ninahitaji nini ili ninunue Bondi hii?

- Unahitaji kuwa na simu ya mkononi (simu ya kawaida)
- Unahitaji kuwa umesajili nambari yako ukitumia akaunti ya simu ya Airtel au Mpesa
- Tumia mfumo wa benki wa PesaLink unaoupendelea na kisha ufuate maagizo
- Unahitaji kufungua akaunti ya CDS ya M-Akiba (hailipishwi!)

15. Je, ninahitaji kufungua akaunti nyingine ya CDS ikiwa tayari ninayo?
Ndiyo. Akaunti yako ya M-Akiba itakuwa tofauti na akaunti za kawaida za CDS unazotumia sasa.

16. Je, nitafunguaje akaunti ya CDS ya M-Akiba?
Baada ya kusajili nambari yako kwa akaunti ya simu ya (Airtel or Mpesa), Piga simu kwa *889# na ufuate maagizo. Utapokea ujumbe wa kuthibitisha kupitia SMS, uliyo na nambari ya akaunti yako ya CDS ya M-Akiba.

17. Nitawezaje kununua Bondi ikiwa ninataka zaidi ya kima cha juu kinachoruhusiwa kila siku?
Utasubiri hadi siku itakayofuata ili ununue. Unaweza kurudia hatua hii kila siku hadi utakapofikisha kiiasi ambacho unataka kuwekeza mradi Bondi ingali kwenye ofa.

18. Nitalipa gharama gani ili kununua bondi ya M-Akiba katika kipindi cha ofa (soko la msingi)?
Katika kipindi cha ofa, bei ya kununua bondi ya M-Akiba italingana na ada za MNO. (Angalia ada za MNO zililizopunguzwa katika tovuti ya M-Akiba- www.m-akiba.go.ke Hakuna matozo yoyote unaponunua ukitumia PesaLink hadi itimiapo tarehe 12 mwezi wa Agosti, 2017. Baada ya tarehe hiyo, huduma hii itaanza kutozwa. Matozo hayo yatategemea kati ya benki moja hadi nyingine.

19. Itanigharimu pesa ngapi kuuza ama kununua bondi baada ya kipindi cha ofa (soko la hisa)?
Bei ya jumla ya kununua na kuuza katika soko la hisa ni 0.335% ya gharama ya shughuli hiyo. Matozo ya kawaida ya PesaLink yatatumika. Ada za kawaida za kuhamisha pesa kutumia simu ya mkononi zitatozwa wakati unaweka au kutoa pesa kwenye akaunti ya simu ya mkononi. Ili kuona maelezo ya kina ya Mapato na Bei ya M-Akiba nenda katika tovuti ya www.m-akiba.go.ke

20. Ninaweza kuchuma pesa vipi nikitumia bondi ya M-Akiba?
Kama mwekezaji utalipwa 10% ya pesa ulizowekeza kila mwaka kwa miaka tatu ijayo. Riba inalipwa baada ya miezi sita. Hii riba ni ya juu ikilinganishwa na huduma zingine za kuweka akiba.

21. Ninaweza kuuza bondi yangu kabla ya kipindi cha miaka mitatu kuisha?
Ndiyo. Unaweza kuuza bondi yako baada ya kumalizika kwa kipindi cha mauzo ya awali kupitia Soko la Hisa la Nairobi (NSE).
Ili uweze kuuza bondi, piga simu kwa *889# na uchague "uza" kisha ufuate maelekezo ili ukamilishe agizo la kuuza. Unaweza kuuza sehemu ya bondi ulizowekeza. Uwezo wako wa kuuza bondi wakati unataka, unasimamiwa na mpango wa mauzo unaofanywa na benki ambayo itahakikisha kuwa umelipwa pesa ulizouzia kati ya saa 9:00 a.m na 3:00 p.m katika siku za kazi isipokuwa likizo.

22. Nitapata vipi pesa zangu nitakapouza bondi ya M-Akiba?
Unapouza bondi yako unapokea pesa papo hapo kwenye akaunti ya simu. Pesa utakazopokea zitajumuisha riba zozote ulizopata lakini tutaondoa ada za akaunti ya simu na ada nyinginezo.

23. Riba yangu itakuwa vipi kama nitauza bondi yangu kabla ya siku ya kulipwa riba?
Riba huhesabiwa kila siku kwa hivyo hutapoteza riba yoyote ikiwa utauza bondi yako kabla ya kipindi cha malipo yanayofuata. Muuzaji atalipwa riba yote kuanzia wakati aliponunua hadi wakati alipouza bondi. Kutokana na ada za akaunti za simu na ada nyinginezo husika, tunapendekeza uuze bondi baada ya siku ya sitini kwanzia tarehe ambayo bondi ilitolewa. Baada ya tarehe hii utapata pesa zote ulizowekeza awali. Ili ufurahie faida kubwa kutoka kwa bondi ya M-Akiba, tunapendekeza usubiri hadi kipindi cha bondi kitakapomalizika.

24. Je ninaweza kununua bondi baada ya ofa kumalizika?
Ndio. Unaweza kununua bondi katika soko la hisa (Soko la Hisa la Nairobi). Unahitaji kupiga simu kwa *899#, uchague "nunua" na ufuate maagizo ili ukamilishe agizo la kununua. Hakikisha kwamba akaunti ya simu yako ina pesa za kutosha kununa kiwango cha bondi unayotaka. Utatozwa ada za kununua. Pia unaweza kutumia Pesalink kununua bondi hii. Nenda kwenye tovuti ya www.m-akiba.go.ke chagua "nunua" na chini ya njia ya kulipa, chagua Pesalink na ufuate maagizo ili kukamilisha shughuli ya kununua Kama ilivyo kwenye swali la tatu.

25. Itachukua muda upi kuanzia wakati nilinunua ama kuuza ili kupata ujumbe wa kuthibitisha?
Mchakato huu hufanyika moja kwa moja. Hata hivyo unaweza kucheleweshwa kutokana na matatizo ya mtandao kulingana na mahali ulipo. Serikali ilichangia jumla ya milioni 150 katika "Toleo Maalum" iliyotolewa Machi 23, ambayo iliwekewa tarehe ya mwisho kama 7 Aprili lakini ilifungwa siku mbili mapema (5 Aprili 2017) kwa kuwa mauzo yalikamilika.

26. Naweza kufuatilia uwekezaji wangu vipi?
Piga simu kwa *899# kisha uende kwa menyu ya 'Akaunti Yangu', utaweza kuona taarifa ya akaunti yako

27. M-Akiba inatofautiana vipi na akiba zingine zinazopatikana sokoni?
M-Akiba ni huduma ya akiba ambayo imeanzishwa na serikali ya Kenya kuhimiza wananchi kuweka akiba ya pesa zao. Wanahakikishiwa riba ya 10% kwa mwaka.

28. Wakala wa hisa ni nani?
Wakala wa hisa ni huluki iliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Hisa (CMA), ambaye hununua na kuuza hisa kama vile bondi, kwa niaba ya wawekezaji.

29. Nitajuaje wakala wangu wa hisa?
Pindi unaponunua Bondi baada ya kujisajili, utakabidhiwa kiotomatiki wakala wa hisa. Zaidi ya hayo, utapokea arifa ya SMS inayoonyesha jina la wakala wa hisa. Wakala huyu wa hisa anaweza kuwa tofauti na wakala wa kawaida wa hisa unayetumia katika hisa nyinginezo.

30. Itakuwaje nikisahau wakala wangu wa hisa?
Ili kujua wakala wako, piga simu kwa *899#, nenda kwa "Akaunti Yangu" na ufuate maagizo yaliyopo.

31. Nitawasiliana na nani ikiwa nina swali lolote linalohusiana na Bondi ya M-Akiba
Unaweza kuwasiliana na Huduma Centre iliyo karibu. Kumbuka tumebadilisha nambari yetu kutoka 0900889000 hadi 0206900020. Tutumie barua pepe kwa info@m-akiba.go.ke au uende kwenye tovuti yetu ya www.m-akiba.go.ke.